

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**614**

**MAARIFA YA JAMII**


**Muda: Saa 3**

**Alhamisi, 10 Mei 2012 asubuhi**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** katika kila sehemu B na C.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Andika majibu yako kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa **Michoro ambayo itachorwa** kwa penseli.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
7. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako **cha kujibia**.



## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Eleza kwa ufupi sababu zilizofanya wapelelezi kutoka mataifa ya Ulaya kuja katika bara la Afrika.
- \*2. (a) Mistari ya kontua ni nini?  
(b) Eleza kazi za mistari ya kontua katika ramani.
3. Fafanua sababu nne zilizosababisha kuzuka kwa vita vya maji maji kati ya mwaka 1905 hadi 1907.
4. Bainisha athari nne zilizotokana na uhusiano wa kibiashara kati ya watu wa Bara la Asia na Pwani ya Afrika Mashariki kati ya karne ya 8 na karne ya 15.
5. Eleza kwa ufupi matokeo hasi ya uhusiano wa kibiashara kati ya watu wa Bara la Ulaya na watu wa Pwani ya Afrika Mashariki kabla ya ukoloni.
6. Eleza kwa ufupi hatua za mabadiliko ya binadamu kwa mujibu wa Charles Darwin.
7. Mji wa Dar es Salaam upo katika longitudo  $45^\circ$  Mashariki. Mji wa Tokyo hupatikana katika longitudo  $120^\circ$  Mashariki. Itakuwa ni saa ngapi katika mji wa Tokyo ikiwa ni saa 2:00 kamili usiku katika mji wa Dar es Salaam?
8. Ainisha tabia nne za nchi zinazopatikana katika ukanda wa nchi za Afrika Mashariki.
9. (a) Taja namna tatu zinazotumika kuonesha kipimo cha ramani.  
(b) Ikiwa sentimeta moja kwenye ramani ni sawa na kilometa kumi na tano kwenye ardhi, kipimo hiki kitaandikwaje katika mfumo wa uwiano?
- \*10. Elezea kwa ufupi namna milipuko ya volkano inavyotokea.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu swali moja (1) kutoka katika kila kipengele.

### Kipengele I: Jiografia

11. Elezea njia tano zinazoweza kutumika kudhibiti athari za ufugaji holela katika mazingira.
12. Fafanua umuhimu wa uoto wa asili katika uchumi wa Tanzania.

### **Kipengele II: Historia**

13. Nchi za bara la Ulaya zilileta ukoloni katika Bara la Afrika katika karne ya 19 kwa sababu za kibinadamu. Jadili.
14. Tathmini athari zilizotokana na biashara ya utumwa katika Bara la Afrika.

### **SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu swali moja (1) kutoka katika kila kipengele.

### **Kipengele I: Jiografia**

15. Fafanua faida tano za kutumia majadiliano kama mbinu ya kufundishia na kujifunzia somo la Jiografia.
16. Eleza kwa kutoa mifano kasoro za kutumia Ziara kama njia ya kufundishia somo la Jiografia.

### **Kipengele II: Historia**

17. Kwa kutumia mifano, eleza sifa tano za zana nzuri za kufundishia somo la Historia.
18. Bainisha njia tano zinazoweza kutumika katika upimaji wa wanafunzi wa somo la historia darasani.